MWONGOZO WA FAMILIA

kuhusu kusaidia vijana kutayarisha maudhui


→ Vidokezo kwa Vijana

common sense networks kwa ushirikiano na YouTube

Utayarishaji wa maudhui ni njia bora ya kuonyesha ubunifu wako, kuwasiliana na kuwapa wengine maoni yako. Tumia vidokezo hivi kuhakikisha kuwa vitu vinafaa, ni salama na vinafurahisha katika mchakato mzima!

KUWA MWENYE MATUMAINI, SI MKAMILIFU


Maudhui yako yatakuwa na athari kwako na kwa mtu yeyote anayeyaona—yafanye yawe ya kuleta matumaini. Fikiria kuhusu jinsi video na maoni yako yatakavyokufanya wewe na watazamaji wako mhisi.



Ni suala la kuwasiliana na watu, si kujilinganisha nao. Usifadhaike kuhusu kuwa mkamilifu au kupata utazamaji na alama za nimeipenda. Tayarisha maudhui halisi na uwe na upekee.

TAHADHARI KUHUSU KUCHAPISHA TAARIFA KWA KUPITILIZA

Baadhi ya vitu si salama kuvichapisha ikilinganishwa na vingine. Jiulize maswali haya ili usaidie kujiepusha wewe na wengine dhidi ya hatari.



FIKIRIA KWA BUSARA

Maudhui yanayovuma na mashindano ni njia ya kufurahisha ya kuonyesha ujuzi wako na kuhisi kuwa unajumuika na wengine. Lakini, baadhi yanaweza kuwa hatari hata ikiwa hatari hiyo si dhahiri kila wakati. Kabla ya kushiriki, fuata hatua hizi tatu:

SITA > TATHMINI HATARI > FANYA UAMUZI

MWONGOZO WA FAMILIA

kuhusu kusaidia vijana kutayarisha maudhui

→ Vidokezo kwa Vijana

common sense networks kwa ushirikiano na YouTube

DHIBITI MAONI YAKO

Maoni na hata ukosoaji ni sehemu ya utayarishaji wa maudhui. Fanya mpango wa jinsi utakavyojibu (au ambavyo hutajibu).



USIPUUZE HISIA ZAKO

Unadhibiti chaguo zako. Tathmini hisia zako wakati wa mchakato mzima.

- *Je, una furaha?* **Huenda unafanya mambo ipasavyo!**
- *Je, una wasiwasi au mashaka?* **Chukua muda kusita na kutafakari.**
- *Je, una mfadhaiko au umekata tamaa?* **Inaweza kuwa ishara kuwa uache au upate usaidizi.**

JITUNZE

Unapotayarisha maudhui, hakikisha kuwa unaweka maslahi yako katika mstari wa mbele...

TAFUTA RAFIKI

Wategemee marafiki, familia na watu wazima wengine unaowaamini.

SAWAZISHA MAMBO

Tenga muda wa vipaumbele na shughuli zingine unazopenda.

TAFAKARI NA UPANGE UPYA

Ulifurahia nini zaidi? Utabadilisha nini wakati ujao?

...na bila shaka, kumbuka KUFURAHIA!